

Nice

**Utambulisho:**

Kwa majina naitwa Nice.

Anwani:

Kwa sasa naishi Goma tangu myaka tatu. Zamani nilikuwa naishi Masisi.

Kuanza kwa vita:

Vita zilianzaka ni nina myaka munane.

Matokeo ya vita:

Zile ma vita ziliniletaya shida/mateso mengi kwangu na kwa jamaa/familia yangu yote kwani tulikimbia na kuishi ndani ya pori/msituni. Wandugu zangu walikuwa katika shida, tulipoteyana/tulitengana, kila mmoja alienda kusikojulikana, watoto wamoja walipoteyanaka na wazazi wao, ndugu zetu waliuawa, nyumba zetu zililunguzwa/zilichomwa moto, wazazi wetu hawakuenda tena mukazi, mushamba kutafuta chakula. Masomo yalisimamishwa, sikusomaka, na ndugu zangu hawakusoma. Kila kitu kilikuwa kimesimama.

Hizo vita ziliniletaya shida sana kukuwa nashituka sana /vitisho vya mara kwa mara, kusahau sana kwani nilikuwa nafikiriya sana kuhusu iyo vita. Kukumbuka/kuwafikiria ndugu zangu waliouawa, mali zetu kuporwa na nyumba zetu zilizolunguzwa/kuchomwa moto na kukumbuka jinsi hatukusoma/ hatukuendelea tena na masomo. Mambo haya yote yamekuwa na hatari(impact) kwenye maisha. Siku tukonasoma/Tunapojifunza sasa, hautasikiya/hatuelewi vizuri kwa sababu unakumbuka hiyo mambo hilipo kuwa kichwani mwako sana.

Hiyo Vita vinaniletaya woga kwa sababu unapokumbuka, huwa na mshtuko ginsi vilipitikana, unaota hiyo vita, huwa na kumbukumbu za matukio ambayo nilipata, hasa nikiwa peke yangu. Nikifika nafasi/sehemu fulani nakutana na mtu amabaye sikumuona/bila kujulishwa kuwepo kwake, nashituka sana, kwa sababu walikuwa natukutana mapori/msituni kwenye tulipokimbilia. Inatosha pia kuona kipande cha mti au kitu kikisogea kwa mbali na kufikiria kuwa ni mtu anayekuja kushambulia ili kuhisi hofu. Tuliporudiya/Tulipofika nyumbani, ulipo lala/sinziya , ilitosha kitu kikaanguka kama chungu kwa mfano au panya kugusa mbao/ubao wa nyumba, unashituka na kuwaza wajambazi wanakuja tena kuwaingiliya/kuwashambuliya kwa kuwauwa. Hasa kama hakukuwa na mtu aliyeniambia kuwa ni kitu kilichoanguka na hiyo ilimaanisha kuwa bado unaweza tena kukimbiya kuelekea porini/msituni na kulala usiku.

Kuna wakati nikiwa darasani mwalimu anafundisha, sikuwa na uwezo wa kusikiya/kuzingatia vizuri chochote hasa nikiukumbuka vipindi nilivyopitia katika vita. Ninapokuwa nyumbani, nataka kusoma au kukagua maandishi yangu (faire l'etude), mambo haya yananiirudia akilini mwangu, siwezi kusoma, na yana athari nyingi kwa mwili wangu na akili yangu kwa sababu ya kushituka mara kwa mara. kusababisha kukosa usingizi usiku kucha na kesho yake husababisha usumbufu darasani.